

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

28 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA – TAREHE 28 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

321. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwa kuwa Hospitali iliyopo haikidhi mahitaji kutokana na uchakavu na ongezeko la watu.

322. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara tatu za Lukoma – Lubalisi, Kalya – Ubanda na Kalya – Sibwe zinazounganisha Mkoa wa Kigoma kupitia Wilaya ya Uvinza.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

323. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA (MTWARA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Mtwara Mjini kwenda Msimbati ambapo kuna Mitambo ya Visima vya Gesi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**324. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS
KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Wananchi wa Ludewa hutegemea Ziwa Nyasa kwa shughuli za uvuvi:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kupeleka Mradi wa Uhifadhi Mazingira Ziwa Nyasa ili kutunza mazalia ya Samaki ambao wameanza kuadimika;

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka fedha pamoja na Wataalam kutoa elimu na kuanzisha Mradi wa Ufugaji Samaki kwenye vizimba ndani ya Ziwa Nyasa ili kuzalisha ajira kwa Wananchi na kuongeza kipato.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**325. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA
ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya ardhi katika Mikoa ya Tabora na Singida ili

Wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa utulivu na amani.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

326. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itafikiria kuweka Mipaka mipya ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ili kutoa maeneo kwa ajili ya Makazi ya Watu na shughuli nyingine za Kijamii kwa kuwa idadi ya Watu wa Same imeongezeka.

327. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Halmashauri ya Wilaya ya Meatu imekumbwa na wimbi kubwa la uvamizi wa Wanyamapori kwenye maeneo ya Vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Maswa na Hifadhi ya Wanyamapori Makao na kusababisha uharibifu wa Mazao na kutishia usalama wa watu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itashughulikia tatizo la uhaba wa Watumishi wa Idara ya Wanyamapori.
- (b) Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya ukosefu wa vitendea Kazi vikiwemo Gari na Silaha.

WIZARA YA NISHATI:

**328. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE
MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme katika Vijiji 28 ambavyo bado havijapata umeme kati ya Vijiji 50 vya Jimbo la Singida Mashariki.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**329. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA
NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni kwa namna gani Serikali imetumia fursa ya Makubaliano ya TICAD kati ya Tanzania na Japan ili kupata Wawekezaji nchini.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

330. MHESHIMIWA DKT. PINDI HAZARA CHANA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Jengo la Utawala la *Central Police* Njombe.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
28 MEI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

